# Je Sisi Ni Marafiki Wa Ulimwengu Au Marafiki Wa Mungu?

## (Are We Friends Of The World Or Friends Of God?)

**Na**

**Ellis P. Forsman**

# Je Sisi Ni Marafiki Wa Ulimwengu Au Marafiki Wa Mungu?

## (Are We Friends Of The World Or Friends Of God?)

**Na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 06, 2011**

# Je Sisi Ni Marafiki Wa Ulimwengu Au Marafiki Wa Mungu?

## Yakobo 4:4

Kitabu cha Yakobo imevuviwa na Mungu na ina dibaji za kinadharia. Kiasi kwamba ni matendo ya kila siku kama matumizi ya ndimi zetu, ikiwasaidia yatima na wajane, kuwa makini wasionyeshe upendeleo, kuwasaidia wenye mahitaji, na kuwarejesha ndugu na dada waliotenda dhambi. Sote tunavutiwa kuwa na marafiki na kuwa rafiki, na Yakobo analiongelea hili pia.

Yakobo anatoa onyo kuhusu marafiki. Anasema, Yak. 4:4, "*Enyi wazinzi hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.*"

Kwa upande mwingine, Yakobo anamtaja Ibrahim aliyekuwa mwaminifu kama mtu aliye "*itwa rafiki wa Mungu.*" Yakobo 2:23, "*Maandiko yale yakatimizwa yaliyonenwa, Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa ni haki; naye aliitwa rafiki wa Mungu.*"

## Inamanisha nini kuwa rafiki wa Mungu?

Yak. 4:4, "*Enyi wazinzi hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.*"

Nilisoma sehemu ambapo kundi la vijana walipaswa kuandika kile walichofikiri kuhusu kuwa rafiki wa ulimwengu inamanisha nini. Hapa kuna mchanganyiko wa majibu yao:

## "Ficha ukweli kwamba wewe ni Mkristo. Acha watu waamini kwamba wewe siyo Mkristo."

Kumbuka Petro. Mat. 26:69-74, "*Na Petro alikuwa ameketi nje behewani; kijakazi mmoja akamwendea akasema, wewe nawe ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya. Akakana mbele ya wote akisema, sijui usemalo. Naye alipotoka nje hata ukumbini, mwanamke mwingine alimwona, akawaambia watu waliokuwako huko, huyu alikuwa pamoja na Yesu Mnazareti. Akakana tena kwa kiapo, simjui mtu huyu. Punde kidogo wale walioudhuria wakamwendea, wakamwambia Petro, hakika wewe nawe u mmoja wao kwa sababu hata usemi wako wakutambulisha. Ndipo akaanza kuapa akisema, simjui mtu huyu. Na mara akawika jogoo.*"

## “Kutembea na marafiki wanaotenda maovu.”

- Kut. 23:2, “*Usiandamane na mkutano kutenda uovu; wala usitie ushahidi wako katika neno lo lote kwa kugeukia kando na kuandamana ili kupotoa hukumu;*”
- 1 Kor. 15:33, “*Msidanganyike; mazungumzo mabaya huaribu tabia njema.*”

## “Kulaani, kunywa pombe, kuvuta sigara.”

- Efe. 4:29, “*Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.*”
- Mit. 23:29-35, “*Ni nani apigaye yowe? Ni nani aliaye, ole? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye mguno?ni nani aliye na jeraha zisizo na sababu? Ni nani aliye na macho mekundu? Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; waendao kutafta divai iliyochanganyika. Usiitazame mvinyo iwapo ni nyekundu; litiapo bilauri rangi yake, ishukapo taratibu; mwisho wake huuma kama nyoka; huchoma kama fira. Macho yako yataona mambo mageni; na moyo wako utatoa yaliyopotoka. Naam utakuwa kama alalaye katikati ya bahari; au kama yeye asinziaye juu ya mlingoti. Utasema wamenichapa wala sikuumia; wamenipiga wala sina habari; nitaamka lini nitazidi kuitafta tena.”*
- *1 Kor. 6:19-20, “Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe;*”

## “Kusikiliza utani mchafu; kuangalia picha za dhambi.”

- Fil. 4:8, “*Hatimaye ndugu zangu, mambo yoyote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.*”

## “Kuvaa mavazi yasiyo ya staha.”

- 1 Tim. 2:9, “*Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani.*”

## “Kuweka vitu mbele ya kanisa (mfano: mchezo wa mpira).”

- Mat. 6:33, “*Bali utafteni kwanza ufalme wake na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*”
- Ebr. 10:24-26, “*Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi yaw engine; bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri mwonavyo siku ile kuwa inakaribia. Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.*”
- Mdo. 20:7, “*Hata siku ya kwanza ya juma tulipokuwa tumekutana ili kuumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane.*”
- 1 Kor. 16:2, “*Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja.*”

## “Kuifuatisha dunia.”

- Rum. 12:1-2, “*Basi ndugu zangu nawasii kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.*”
- 1 Yoh. 2:15, “*Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia, mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake.”*
- Yak. 4:4, *“Enyi wazinzi hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu? Basi kila atakaye kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu.*”

## “Taratibu unaanza kukubali ambacho dunia inafanya kana kwamba yote ni sahihi.”

- Ebr. 2:1, “*Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa.*”

## “Inamana gani kuwa rafiki wa Mungu kama Ibrahimu alivyokuwa?

## Mwamini Mungu.

Ibrahimu alifanya hivyo (Yakobo 2:23). Tunapenda kuwa na marafiki ambao tunaweza kuamini. Haiwezekani Mungu aseme uongo na Ibrahimu alijua. Hivyo basi, anaweka tumaini lake kwa Mungu na kufanya alichoambiwa bila kujali ambacho Mungu amemwambia afanye. Mungu alimuita rafiki yake.

## Mtii Mungu.

Ebr. 11:8, “*Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika, atoke aende mahali pale atakapopapata kuwa urithi; akatoka asijue aendako.*”

Haiwezekani kuwa rafiki wa Mungu pasipo kutii kile anachosema. Je umetubu na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi? Kama siyo, unadhani unaweza kuwa rafiki wa Mungu?

## Mwabudu Mungu.

Tena na tena inasemwa katika Mwanzo 12-15 kwamba “*alijengaa madhabahu kwa ajili ya Yehova.*” Ni vizuri kiasi gani kumwabudu Yehova! Ibrahimu alifanya hivyo na akaitwa rafiki wa Mungu.

## Kuwa na hakika kwamba Mungu anaweza kutimiza ahadi zake.

Ibrahimu alikuwa na uhakika thabiti na kile alichoahidiwa na Mungu, alikuwa tayari pia kutenda.

Rum. 4:21, “*Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*”

Sawa na jinsi Mungu alivyotimiza ahadi ya mwana kwa Ibrahimu, hivyo Mungu ameahidi uzima wa milele kwa wote wanaomtii. Mungu anaweza!

## Hitimisho

Chagua kuwa rafiki wa Mungu na siyo rafiki wa ulimwengu!